# LEARNING BY EAR 2011

## “The Promised Land - A Story of African Migration to Europe”

## EPISODE TEN: “Two Faces of Migration”

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITORS: Katrin Ogunsade, Klaus Dahmann**
**PROOFREADER: Pendo Paul**

**KISUAHELI: Eric Ponda**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: LINDA HAVING SUPPER WITH PARENTS**

- **Linda (f, 20)**
- **Mr. Maraga (m, 60)**
- **Mrs. Maraga (f, 55)**

**SCENE TWO: LINDA, CHIVASI AND FRIENDS AT A LOCAL PUB**

- **Linda (f, 20)**
- **Chivasi (m, 22)**
- **Dora (f, 20)**

- **2-4 friends (m +f, 18-25)**

## SCENE THREE: FARAHANI CROSSES INTO EUROPE ILLEGALLY

- **Farahani (m, 19)**
- **Frontex guard (m, 40)**
- **Human Trafficker (m, 45)**
- **3-5 migrants (mainly male, age not important)**

## INTRO:

Hujambo msikiiaji na karibu kwenye mfululizo wa vipindi vya Noa Bongo Jenga maisha yako. Hii ni sehemu ya kumi katika hadithi hii, **“Ardhi ya Ahadi- kuhusu Waafrika kuhamia Ulaya.”** Katika hadithi hii tunaangazia wahamiaji halali na wasio halali kutoka Afrika kuelekea Bara Ulaya, ambalo linachukuliwa na wengi kama Ardhi ya Ahadi. Linda amekuwa akifanya kazi katika klabu moja ya usiku inayomilikiwa na mzungu. Kazi aliyotafutiwa na rafiki yake Florence. Tukirudi nyumbani Afrika, Chivasi hajazungumza na mchumba wake kwa muda mrefu, na ameanza kuwa na wasiwasi. Anakwenda kuwatembelea wazazi wa Linda kumjulia hali ya Linda. Akiwa nyumbani kwa wazazi wa Linda, anafahamu matatizo ya kifedha yanayowakumba wazazi wa Linda, baada ya wote kuachishwa kazi. Chivasi anapewa nambari ya simu ya Florence, rafiki mkubwa wa Linda, lakini anapojaribu kumpigia, anashangazwa na jinsi Florence anavyomjibu kwa ujeuri, na kumtaka asahau kabisa mambo ya mchumba wake Linda na kisha kukata simu! Ni changamoto kubwa kwa Linda! Na anaamua kuchukua likizo na kurudi nyumbani. Wakati huo huo, Rafiki wawili Farahani na Sule kutoka Afrika Kaskazini wametofautiana kuhusu suala la kuondoka nchi yao inayokumbwa na mzozo wa kisiasa. Farahani anaamua kujaribu tena bahati yake ya kuhamia Ulaya- na kumuacha nyuma rafiki yake Sule. Katika kipindi cha Leo, **“Sura mbili za**

**Wahamiaji”,** tunafungua pazia nyumbani kwa Familia ya Mzee Maraga, ambako Linda amewasili nyumbani ghafla kutoka Ulaya bila ya taarifa kwa mtu yoyote. Wazazi wanamshangaa binti yao jinsi alivyobadilika. Mengi zaidi endelea kusikiliza tunapoungana nao baada ya chakula cha jioni.

**SCENE ONE: LINDA HAVING SUPPER WITH PARENTS**

1. **SFX: EVENING ATMO/ MOSQUITOES BUZZING**

2. **LINDA:** **(slaps her hand)** Ah! Hawa mbu wanakiu sana cha damu!

3. **MRS. MARAGA:** **(takes a deep breath)** Bado siamini macho yangu kwamba Linda amerudi!

4. **MR. MARAGA:** **(laughs)** Wakati nilipofungua mlango na kukuona umesimama mlangoni na mizigo yako, nilifikiri naota. Bado hatuamini!

5. **LINDA:** Baba, Mama, tafadhali naomba mfunge madirisha? Mbu wanazidi kuingia.

6. **MRS. MARAGA:** Bila shaka, unavyotaka binti! Hapa ni nyumbani kwako Linda. Hebu tueleze habari za huko Ulaya, masomo yako yanavyoendelea, kazi na rafiki wako wote. … Ama kwa kweli umebadilika!

7. **MR. MARAGA:** Amebadilika sana, lazima unapata mshahara

mkubwa sana huko Ulaya – Mavazi yako yanapendeza, viatu, simu mpya, Laptop saa pia ni mpya…

**8. MRS. MARAGA:** **(cuts him short)** Kwa ufupi ni Linda Mpya! Enhe! hebu tueleze umekuwa ukifanya kazi gani kuweza kununua vitu hivi vyote?

**9. LINDA:** Ninafanya kazi katika sekta ya kutoa huduma. Na huko Ulaya kazi hizi huwa zinalipa vizuri sana. Sahamani lakini ningependa kukutana na rafiki zangu!

**10. MR. MARAGA:** **(shy)** Bila ya samahani. Mambo yamebadilika sana hapa siku hizi Linda… tangu tuachishwe kazi! Umeme umekatwa kwa sababu ya kushindwa kulipa ankara. Ndio sababu tunaishi katika giza.

**11. SFX: HANDBAG BEING OPENED**

**12. LINDA:** Shikeni hizi euro 500 – Nadhani zitatosha kwa sasa?

**13. NARRATOR:** Linda, sasa ni tajiri, na mkarimu sana. Lakini bado hajawaeleza wazazi wake kazi anayofanya kupata pesa hizi zote. Kwa furaha waliyonayo, wazazi wake hawaoni kuna haja ya kumuuliza. Baadaye, Linda anaungana na rafiki wake wa zamani katika klabu moja ya mtaani, ambayo zamani hangethubutu kukanyaga. Miongoni mwao ni mchumba wake Chivasi na rafiki yake Dora waliosoma pamoja .

**<u>SCENE TWO: LINDA, CHIVASI AND FRIENDS AT A LOCAL PUB</u>**

14. **SFX: LOCAL PUB ATMO WITH AFRICAN MUSIC PLAYING IN BACKGROUND**

15. **LINDA:** Ohh, Nafurahi sana nimerudi! Na kukutana tena nanyi. Pia nimefurahi sana kwa kufika kwenu licha ya notisi ya muda mfupi.

16. **DORA:** Yote haya ni kwasababu ya mtandao wa Facebook.

17. **CHIVASI:** Bado siamini kwamba umerudi! Nilidhani ni utani tu “Eti niko nyumbani kwa muda wa wiki moja – tunaweza kukutana usiku”! Nilidhani, mimi ningekuwa mtu wa kwanza kunijulisha kama warudi nyumbani.

18. **DORA:** Wow! Linda, ume… umependeza. Kwani huko Ulaya watu wanakula nini? Kila mtu anayekwenda Ulaya hurudi akiwa amebadilika kabisa, mrembo afya nzuri, na hadhi yake pia.

19. **CHIVASI:** Na pesa pia.

**LIGHT LAUGHTER AGAIN**

20. **LINDA:** Ah, sasa niseme nini? Huko maisha ni mazuri! Nasomea somo ninalolipenda zaidi, mbali na

kufanya kazi wakati wa muda wangu wa ziada na kulipwa vizuri. Kwa ufupi, maisha yangu ni mazuri huko! Leo mimi ndio nagharamia kila kitu, chakula na vinywaji, kwa hivyo kila mmoja shibe yake!

**21. SFX: HUGE APPLAUSE, WHISTLES AND “WOWS” FROM CROWD**

**22. DORA:** Linda, pia mimi nataka kuja kuishi huko! Unaweza kunisaidia kunitafutia familia ambayo iko tayari kunipokea huku nikifanya kazi, au kupitia mpango wa masomo wa kubadilishana wanafunzi.

**23. LINDA:** Dora, si rahisi kama unavyofikiria!. Ukiwa na viza kila kitu….

**24. CHIVASI:** Lakini wewe ulifaulu! Na kusema kweli sikudhania kwamba baada ya muda mfupi ungeweza kufanya kazi na kupata pesa za kutosha kujilipia nauli ya ndege kurudi nyumbani. Au kuna mtu amekulipia nauli….?

**25. DORA:** Mmm… Tayari naona Chivasi ameanza kuwa na wivu!

**26. CHIVASI:** Wivu? Mimi? Sina sababu yoyote ya kuwa na wivu! Nampenda Linda na nitafanya kila niwezalo kuwa naye, hata ikiwa ni kuivuka bahari!

**27. LINDA:** Una uhakika? Kweli unaweza kufanya hivyo kwa sababu yangu? Ningefurahi sana kuishi na wewe

Ulaya!

**28. DORA:** Sawa, tosha- tumekuja kusherehekea na sio kuzungumzia mipango yenu ya baadaye! Hebu sasa twendeni tucheze.

**LOUD REACTIONS FROM LINDA’S CROWD OF FRIENDS**

**29. NARRATOR:** Huku Linda na rafiki zake wakicheza na kusherehekea kwa mualiko Linda, upande mwingine katika ufuo wa bahari huko Afrika Kaskazini, Farahani hatimaye amefikia uamuzi. Yeye pamoja na wahamiaji wengine wasio halali wanamlipa mlanguzi wa watu kuwasafirisha hadi Ulaya kwa mashua ndogo, na tayari wamefika kati kati ya bahari ya Mediterania ambako wanakumbwa na mawimbi makali. Maombi yao ni kwamba safari hii mashua yao haitakamatwa na walinzi wa mpakani huko Ulaya na kurudishwa nyumbani. Lakini ole wao hawana habari kuhusu yale yanayowasubiri. Wanakodolewa na hatari kubwa zaidi. Endelea kusikiliza.

**SCENE THREE: FARAHANI CROSSES INTO EUROPE ILLEGALLY**

**30. SFX: HIGH WAVES CRASHING DOWN ONTO A BOAT**

**31. SMUGGLER:** Sawa nimejaribu kadri ya uwezo wangu kuwakwepa walinzi wa mpakani. Sasa tumevuka na kuingia maji ya bahari ya Ulaya na tumesalia na kilomita chache tu kufika ufuoni. Siwezi kwenda zaidi ya hapa, ni shauri yenu sasa! Mnaona ufuo wa bahari pale, kila mmoja sasa ni ole wake, atumie ujuzi wake wa

kuogelea hadi ufuoni au hadi utakapookolewa baharini.

**32. SFX: UPROAR FROM AN ANGRY GROUP OF MIGRANTS**

**33. FARAHANI:** Huwezi kutufanyia hivi! Tumekulipa pesa za safari kamili, mbona unatuacha katikati ya Safari!

**34. SMUGGLER:** Tokeni haraka! Sina muda wa kupoteza! Wakitupata hapa sote tutarejeshwa nyumbani. Kumbuka: Usithubutu kuwaambia unakotoka isipo kuwa tu kama nchi yake inakumbwa na vita. Sasa lazima sasa nianze safari ya kurudi. Muamue haraka. Kuogelea hadi ufuoni au nimurudishe Afrika.

**35. SFX: PEOPLE DIVING INTO THE SEA - PANIC AND CRYING**

**36. FARAHANI:** Mungu nisaidie.…

**37. SFX: FARAHANI JUMPS INTO THE SEA - SWIMMING AND GASPING IN THE WATER**

**38. NARRATOR:** Bila kupoteza wakati Farahani anajirusha baharini na kuanza kung’ang’ana na mawimbi makali yanayozidi kumsukuma nyuma. Kila upande ni makelele ya wahamiaji wenzake wanaotapatapa wasife maji. Ombi lake kubwa sasa ni aweze kuogolea hadi ufuo wa bahari ya Ardhi ya Ahadi. Hatahivyo, lakini kinyume na alivyotarajia, Farahani anaogelea kwa muda wa saa mbili, bila ya kufika ufuoni,

unaoonekana kuzidi kusonga mbali kila wakati. Huku akionekana kuishiwa na pumzi, anasikia sauti ya mashua ikimkaribia, na sauti ya Mzungu ikiita…

**39. FRONTEX GUARD:** **(via megaphone)** Chukua hii jazi ya kuogelea.!

**40. SFX: SHIP ENGINE REVVING IN THE SEA**

**41. FRONTEX GUARD:** Sawa mtoe! Mvute tumweke kwenye mashua.

**42. FARAHANI**: (**breathing heavily**) Wewe… wewe ni nani?

**43. FRONTEX GUARD:** Sisi ni maofisa wa ulinzi wa mpakani Baharini kutoka shirika la Frontex, shirika linalolinda usalama baharini kwenye mpaka wa Bara la Ulaya. Sasa umevuka mpaka na kuingia eneo hili kinyume cha sheria. Wewe ni nani na unatoka wapi?

**(silence)**

**44. FRONTEX GUARD:** Unatoka Afrika, Asia, au Mashariki ya kati? Wewe ni asili ya Mwarabu, sivyo?

**(silence)**

**45. FRONTEX GUARD:** Je uko na wenzako ?

**46. FARAHANI:** **(nodding)** Mmmh. Mmm-hmm.

**47. FRONTEX GUARD: (via megaphone)** Ndio wako wengine! Kuna wengine wengi baharini! Tuendelee kuwasaka… tufanye haraka hatuna muda wa kupoteza!

**OUTRO:**

Ndoto ya Farahani hatimaye inaelekea kutimia. Ingawa amelowa, ameshikwa na baridi kali, njaa, kiu na kuchoka, amefanikiwa kuingia Ulaya. Je nini hatima yake huko Ulaya? Na je! Safari ya Linda nyumbani ina maana gani kwa familia na rafiki zake? Ungana nasi kwa sehemu ya 11 ya mchezo huu Ardhi ya Ahadi. Pia ukipenda kusikiliza tena kipindi hiki unaweza kutembelea mtandao wetu wa dw.de/destinationeurope. Hadi wakati mwingine kwaheri kwa sasa.